

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHURI YA WILAYA YA IRINGA



TANGAZO

ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI USHURU WA MAZAO YATOKANAYO NA MISITU,
MADINI YA UJENZI, MAEGESHO YA MAGARI NA USHURU WA PIKIPIKI KATIKA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

TAREHE: 26/09/2017

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa anawatangazia Wafanyabiashara wote, Vikundi vilivyosajiliwa, Makampuni na Watu binafsi wenye uwezo na sifa za kutoa huduma kama ilivyo elekezwa kwenye jedwali hapa chini kwa kipindi cha mwaka fedha 2017 /2018 kwa kuleta maombi yao:

NAMBA YA ZABUNI	ENEO ILIPO	MAELEZO
LGA/026/2017/2018/S/39	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Ukusanyaji ushuru wa mazao yatokanayo na misitu
LGA/026/2017/2018/S/40	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Ukusanyaji ushuru wa madini ya ujenzi
LGA/026/2017/2018/S/41	Ifunda, Tanangozi, Ugwachanya, Kidamali, Ndiwili, Kalenga Migoli na Tungamalenga	Ukusanyaji ushuru wa maegesho ya magari na ushuru wa pikipiki

MASHARTI YA WAOMBAJI:

1. Kila mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania.
2. Muombaji aambatishe usajili wa TIN (au VAT)
3. Muombaji anatakiwa awe na Leseni husika.
4. Muombaji aambatishe uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax Clearance Certificate) ya mwaka 2016/2017

5. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonyesha Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement) ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyo idhinishwa na kuthibitishwa na Meneja wa Benki ya tawi husika.
6. Muombaji aambatishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakaye husika na zabuni hii.
7. Taarifa ya madeni yake yote (kama yapo) anayo daiwa na watu binafsi, Benki na Halmashauri hii au nyingine katika Tanzania
8. Muombaji anatakiwa kutokuwa na mgogoro wowote na Halmashauri.
9. Muombaji atakayepata kazi atatakiwa awasilishe alipe/ (dhamana) fedha taslimu zinazolingana na mawasilisho ya miezi mitatu (3). Fedha hizi atarudishiwa baada ya mkataba kuisha endapo atakuwa hadaiwi.
10. Muombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Shilingi ishirini elfu tu (TZS. 30,000.00) kwa kila ombi la Mzabuni na kupewa stakabadhi pamoja na kabrasha la Zabuni ambalo utatakiwa kulijaza na kulirudisha kabla ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ada ya maombi hairudishwi.
11. Maombi yafungwe katika bahasha kwa lakiri (Seal) katika bahasha mbili (2) moja halisi na moja nakala na kuonesha namba za zabuni, na kuwasilisha katika, **“OFISI YA KITENGO CHA MANUNUZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA MAKAO MAKUU, S.L.P. 108, IRINGA”**
12. Maombi yaandikwe kwa, **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA, S.L.P. 108, IRINGA.**
13. Mwombaji atatakiwa kutoa mchanganuo wa mapato na matumizi kuonesha chanzo/vyanzo vya mapato na maoteo yake yaliyofanyiwa utafiti na upembuzi yakinifu kabla ya kujaza zabuni.
14. Muombaji ataje kiasi (*sahihi* na *halisi*) atakachoilipa Halmashauri kutokana na mchanganuo wake.
15. Maombi ambayo hayatazingatia masharti yaliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa.
16. Waombaji wote wanakaribishwa kufika wenyewe au kutuma wawakilishi wenu siku ya ufunguzi. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya Iringa.
17. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09/10/2017 saa nne kamili asubuhi (4.00) na zabuni zitafunguliwa baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Iringa.

Robert M.Masunya
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

